ORGANISATION INTERNATIONALE DE la francophonie

Kutiliwa matumizi ya

LUGHA NYINGI

Katika mashirika ya kimataifa

Kutekeleza
Tofauti za lugha

Nathan

OFISI YA UCHUNGUZI WA KIFARANSA

Yaliyomo

Ulimwengu wa lugha nyingi

Baadhi ya maeneo makubwa ya lugha ulimwenguni 5
Mapiganio ya Francofonia juu matumizi ya lugha nyingi 10
Faida zinazotokana na kutiliwa matumizi ya lugha nyingi 11

Desturi nzuri

Kuhusu tafsiri na ufafanuzi 16
Kuhusu kuwaandikisha watu kazini 18
Kuhusu mawasiliano na habari 19
Katika matendo ya pamoja 19
Katika ofisi za kuchua uamzi 20

Habari za manufaa

Siku za lugha 22
Mawasiliano 24
Mfumo wa lugha wa mashirika makubwa ya kimataifa 25
Nchi na serkali memba za Francofonia 28
Mwongozo wa Francofonia Kuhusu matumizi ya
lugha ya kifaransa katika mashirika ya kimataifa 29

© Éditions Nathan, Paris, 2013
ISBN : 978-2-09-882672-4

Kitendo chetu kinajitia katika mbinu kuhusu lugha zote ; ni kile cha matumizi ya lugha nyingi kama chombo cha demokarasia ya mawasiliano ya kimataifa. Hakika kuvunja heshima ya usawa wa lugha rasmi na zile za kazi ndani ya mashirika ya kimataifa ni, bila shaka, kutaka kuzuru na kuchafua hali ya mazungumzo na ya ushirikiano vinavyo kuwa misingi ya matumizi ya lugha nyingi yanayodaiwa na Francofonia

Abdou Diouf
Katibu mkuu wa Franconfia, 2008

Jambo muhimu la mawasiliano ya amani kati ya mataifa, matumizi ya lugha nyingi yana lazima kubwa sana... Yakiwezesha kuvumiliana, matumizi ya lugha nyingi yanawezesha pia kuweko ushirikiano wa kweli na mkubwa kati ya watu wote katika taratibu ya kazi ya Shirika, na vilevile nguvu kubwa zaidi, matukio bora na kujihusisha kwa nguvu zaidi. Matumizi ya lugha nyingi yanapashwa kulindwa na kupatiwa nguvu katika matendo tofauti... kwa nia ya kugawana na kuwasiliana.

Ripoti ya Katibu mkuu
Ban Ki Moon
Kuhusu matumizi ya lugha nyingi, 2007

Ulimwengu wa lugha nyingi

Baadhi ya maeneo makubwa ya lugha ulimwenguni

Eneo la matumizi ya kiingereza

Hali : Kiingereza ni lugha rasmi ao moja ya lugha rasmi ya nchi 54 zinazopatikana katika mabara yote. Jumuiya ya Madola ni shirika lenye kukusanya nchi zenye kutumia kiingereza.
Watu : Karibuni, miliardi 1.8 za wakaaji.
Hali katika mashirika :
Kiingereza ni lugha rasmi na ya kazi katika mashirika yote ya kimataifa (isipokuwa tu katika Umoja wa kimataifa wa huduma za posta) na vilevile katika mashirika ya kimkoa (isipokuwa kama mashirika haya yanatungwa tu na nchi ao maeneo madogo kijeografia).

Wazungumzaji : Kwa jumla, kunahesabiwa, karibuni, milioni 500 ya watu wanaozungumza kiingereza (hesabu nyingine zinafikia hata miliardi moja). Kiingereza ni lugha ya pili ya mama inayozungumzwa zaidi ulimwenguni.
Mafunzo yake : Idadi ya watu wanaojifunza kiingereza ulimwenguni inafikiriwa kuwa miliardi 2. British Council inapatikana katika nchi 110 ulimwenguni.

Eneo la matumizi ya kiarabu

Hali : Kiarabu ni lugha rasmi ao moja ya lugha rasmi katika nchi 22. Shirika la kiarabu kuhusu Elimu, Utamaduni na Sayansi (ALESCO) linakusanya nchi zinazozungumza kiarabu.
Watu : Wanahesabiwa watu milioni 350 wanaozungumza kiarabu.
Hali katika mashirika : Kiarabu ni lugha rasmi na/ao ya kazi ya mashirika makubwa ya Umoja wa Mataifa na ya Taasisi zake maalum, na vilevile ya mashirika makubwa ya kijimbo ya kiarabu (Ligi ya kiarabu, OCI, ALESCO).
Wazungumzaji : Wanafikiriwa kuwa milioni 250.
Kiarabu, ao vema zaidi, aina tofauti ya lugha hii zinachukua nafasi ya nne ya lugha zinazozungumzwa zaidi ulimwenguni, tukizingatia tu watu wanayo lugha hii kama lugha ya kwanza.
Mafunzo yake : Moja ya sababu kubwa ya kusambaa kwa kiarabu ni dini ya kiislamu ambayo iliwasukuma watu wengi kutaka kuijuwa na hata kuisoma. Ni hivi, katika baadhi ya nchi, kiarabu kinatumiwa tu katika shuruli za kidini (Bangladeshi, Indonezia, Irani, Pakistani, Uturuki).

Eneo la matumizi ya kifaransa

Hali : Kifaransa ni lugha rasmi ao moja ya lugha rasmi katika nchi na serkali 35 za Shirika la kimataifa la Francofonia. (O.I.F.)
Watu : Kunakadiriwa kuwa watu milioni 350 katika maeneo yale.

Hali katika mashirika : Kifaransa ni lugha rasmi na ya kazi ya taaasisi maalum za Umoja wa mataifa na pia ya tume zote za kijimbo na taasisi za mfumo wa Umoja wa mataifa (isipokuwa tu Benki kuu la dunia na Fuko kuu la kimataifa), pia ya mashirika mane ya kiamerika ya ndani (BID, COPA, FIPA, OEA), ya mashirika mawili ya kimkoa na ya Umoja wa Ulaya, na vilevile ya karibuni mashirika yote ya kimkoa ya kiafrika (UEMOA, BAD, CEDEAO, UA).

Wazungumzaji : Watu milioni 220, ulimwenguni, wanaweza, bila shaka, kuangaliwa kama wazungumzaji wa kifaransa ; hesabu hii haiihusu sehemu kubwa ya watu wasiojua kusoma na kuandika wanaoishi katika nchi za kusini ambao wanaweza kuzungumza ao kusikia katika kifaransa (lakini hawawezi kukisoma ao kukiandika).

Kifaransa ni **lugha ya tano inayozungumzwa** zaidi ulimwenguni.

Mafunzo yake : Inahesabiwa watu milioni 116 wanaojifunza kifaransa (ambao karibuni nusu kama lugha ya kigeni). Lugha ya ulimwengu, kifaransa kinatumika kama lugha ya mafunzo, lakini pia kama mojawapo ya lugha haba zinazofunzwa karibuni katika mabara yote. Kikipatikana katika mifumo ya masomo na ya vyuo vikuu, kifaransa kinakuzwa na kufundishwa kwa kupitia mitandao ya nchi ya sehemu mbili ao ile ya sehemu nyingi ao tena ile isiyokuwa ya kiserkali ; mmoja wapo ikiwa ni taasisi za kifaransa na Ushirikiano wa kifaransa ambayo zaidi ya shule zao 1100 zinapatikana katika zaidi ya nchi 130.

Eneo la matumizi ya kihispania

Hali : Kihispania ni lugha rasmi ao moja ya lugha rasmi katika nchi 20.

Shirika la nchi za Amerika ya kusini kuhusu Elimu, Sayansi na Utamaduni (OEI) na ofisi za Katibu wake mkuu (SEGIB) zinakusanya nchi zinazozungumza kihispania.

Watu : Jumla ya nchi ambamo huzungumza kihispania zina karibuni watu milioni 380.

Hali katika mashirika : Kihispania ni lugha rasmi ao/na ya kazi ya mashirika maalum ya Umoja wa mataifa na ya taasisi zake maalum, ya mashirika mawili ya kimkoa ya kiafrika (SADC, UA), ya Umoja wa Ulaya na ya, karibuni, jumla ya mashirika yote ya kimkoa ya Amerika (ALENA, AEC, MERCOSUR).
Wazungumzaji : Milioni 450 (ambao 329 wanayo kama lugha ya mama).
Mafunzo yake : Watu karibuni milioni 14 wanajifunza kihispania kama lugha ya kigeni (milioni 5 wapo Brazilia). Kwa kupitia vituo vyake vinavyopatikana ulimwenguni kote, Taasisi ya Cervantes inashurlika na kukuza na mafundisho ya lugha ya kihispania, pia na usambazaji wa utamaduni wa kihispania na ule wa kimarekani-kihispania.

Eneo la matumizi ya kireno

Hali : Nchi nane kunako mabara mane zinatumia kireno kama lugha rasmi. Kireno ni pia moja ya lugha rasmi katika jimbo la kiutawala wa pekee wa Macao(pamoja na kichina) na ya Timori ya mashariki (pamoja na kitetumi). Jumuiya ya nchi za kireno (CPLP) inakusanya nchi zenye kutumia kireno.
Watu : Watu katika maeneo haya hufikiriwa kuwa milioni 215.
Hali katika mashirika : Kireno ni lugha rasmi ya Baraza kuu la UNESCO, ya mashirika mengi ya kimkoa ya kimarekani (MERCOSUR,OEA, UNASUR, EIA), ya Umoja wa Ulaya, lakini pia ya mashirika matatu ya kijimbo ya kiafrika (UA, SADC, na CEDEAO).
Wazungumzaji : milioni 240.
Mafunzo yake : Taasi ya Camoes inahusika na upanuzi wa lugha na utamaduni wa kireno katika nchi za kigeni.

Eneo la matumizi ya kirusi

Hali : Kirusi ni lugha rasmi ya nchi nne.
Watu : Hukadiriwa watu milioni 175 katika eneo hili.
Hali katika mashirika : Kirusi ni lugha rasmi na /ao ya kazi ya Umoja wa mataifa na taasisi zake maalum, na pia ya mashirika ya kimkoa ya Ulaya na Asia (OSCE, Baraza la Ulaya, CEI, OCS).
Wazungumzaji : Watu kati ya milioni 300 na 350, ulimwenguni, hasa katika Ulaya ya mashariki na Asia. Kirusi ni lugha ya mama ya watu milioni 200 (ambao milioni 70 huishi nje ya Urusi).
Mafunzo yake : Kati ya watu milioni 100 na 150 wanajifunza kirusi duniani.

Eneo la matumizi ya kichina

Hali : Kichina ni lugha rasmi ao moja ya lugha rasmi ya nchi ao tarafa tano (Uchina, Hong-Kong, Macao, Singapuri na Taiwani).
Watu : Hufikiriwa kuwa watu miliardi 1,4 kwenye eneo hili.
Hali katika mashirika : Kichina ni lugha rasmi na /ao ya kazi ya Umoja wa mataifa na taasisi zake maalum, na pia mashirika yake mawili ya kimkoa ya Asia (ASEAN na OCS).
Wazungumzaji : Karibuni watu miliardi moja na milioni 445 wanazungumza lugha za “kichina ulimwenguni” wakiwemo karibuni milioni 836 kwa kimandirini. Basi, kutokana na hesabu, kichina ni lugha inayoshika nafasi ya kwanza za lugha zenye kuzungumzwa ulimwenguni.
Mafunzo yake : Kulingana na hesabu rasmi za kichina, kuna karibuni watu milioni 40 wanaojifunza kichina kama lugha ya kigeni (wanatarajiwa kufikia milioni 100 katika mwaka wa 2020). Katika nchi za magharibi, vyuo vikuu 700 vinatoa mafunzo ya kichina. Taasisi ya *Confucius* zinazopatikana katika miji mikubwa ulimwenguni zinafundisha kichina na zinachangia hivi katika kusambaaza utamaduni wa kichina.

Mapiganio ya Francofonia Juu ya matumizi ya lugha nyingi

Ikiwa kama lengo la kwanza la Francofonia ni kudumisha, ndani ya maeneo yake, matumizi ya kifaransa kama lugha ya mawasiliano, ya ushirikiano na ya mafundisho, inakusudia, kwa wakati uleule, kujiingiza katika vita kubwa : ***ile ya kukubalisha kuweko tofauti za tamaduni na za lugha***.

Matumizi ya Lugha nyingi sababu ya demokrasia

Mnamo mwezi wa novemba 1998, kulifanyika pale Geneva, kwa ombi la Francofonia, kongamano lililowakusanya wafanyakazi wa kimataifa pamoja na mabalozi juu ya kuzungumzia kuhusu swala la kifaransa na matumizi ya lugha nyingi katika mikutano ya mashirkia ya kimataifa.

Lengo lilikuwa kukumbusha umuhimu wa kuweko tofauti za lugha kama sababu ya kuyapatia demokrasia mawasiliano ya kimataifa.

Miongoni mwa mapendekezo yaliyochukuliwa wakati ule kulikuweko kuundwa kwa tume ya uchunguzi na ya kukinga matumizi ya lugha nyingi katika mashirika ya kimataifa ili kuwekesha heshima ya hali ya lugha ya kazi na umuhimu wa kuyagusisha zaidi mashirika ya nchi zinazozungumza kiingereza, kireno na kihispania juu ya kuzingatia lugha kama sharti kwa kuwaandikisha watu kazini.

Tofauti za tamaduni, sharti ya utandawazi sawa, wenyi kushikama na wa amani

Katika mwezi wa juni 2001, pale Cotonou, Mkutano wa tatu wa mawaziri wa Francofonia kuhusu utamaduni ulitamani kuundwa chombo cha kisheria cha kimataifa wakitilia mkazo umuhimu wa tofauti za kitamaduni na lazima ya kukuza na kukinga viwanda vya tamaduni.

Swala hili lilibakia kama shuruli ya Francofonia ambayo ilililingiza katika mbinu yake kwa kipindi cha myaka kumi, iliyokubaliwa katika kikao cha X cha viongozi wa nchi na

serkali (Ougadougou, novemba 2004). Kikao hiki kinajulisha kazi kubwa ya Shirika la kimataifa la Franconfonia (OIF), zikiwemo kuikuza lugha ya kifaransa na kukubali kuweko tofauti za kitamaduni na za lugha.

Ni kwa wakati ule Francofonia ilifanya nguvu sana juu ya kukubaliwa Mkataba juu ya kukinga na kukuza na UNESCO tofauti za maonyesho ya kilugha, kusudio lililopigiwa kura na Baraza kuu mnamo mwaka wa 2005 na kuanza kutekelezwa mwezi wa tatu 2007 ;

Heshima ya lugha rasmi katika mashirika ya kimataifa, alama ya usawa na ya nguvu

Mnamo mwezi wa septemba 2006, pale Bucaresti, kikao cha XI cha viongozi wa nchi na serkali wa Francofonia kilikubali *Kitabu cha Mwongozo kuhusu matumizi ya kifaransa katika mikutano ya mashirika ya kimataifa*. Ikiwa kama Nchi na Serkali, memba wa Francofonia, zilikubali pendekezo hilo, haikuwa tu kwa kukinga lugha ya kifaransa, lakini ilikuwa sababu walipima umuhimu unaotokana na vita juu ya matumizi ya lugha nyingi na heshima ya hali ya lugha rasmi na ya kazi ndani ya mashirika ya kimataifa.

Faida zinazotokana na kutiliwa matumizi ya lugha nyingi

Kunako ofisi za kimataifa ambamo, kufwatana na hali zao, zinapashwa kushurlika na mazungumzo na mapatanisho, faida zinazotokana na swala la lugha za mawasiliano ni kubwa. Hakika, inahusika na mwendesho wa nguvu na wa kidemokrasia wa mashirika ambao haungeliwezekana bila kuweko hata kidogo hali ya usawa katika kupata habari na kuchukua sauti kwa kutumia lugha inayoeleweka vizuri.

Demokrasia

Ikikubaliwa ya kwamba kila lugha inaficha ndani mwake mtazamio wa ulimwengu, basi matumizi ya lugha moja tu ni pingamizi kwa jaribio la kuweko tofauti za kitamaduni na maoni ; vilevile matumizi yale yanawapunguzia raia uwezekano wa kupata habari zenye kuwahusu. Basi, heshima kwa matumizi ya lugha nyingi ni nguzo dhidi ya kuweko fikra moja tu. Inachangia katika kuyapatia demokrasia mawasiliano ya kimataifa.

Usawa

Katika shirika la kimataifa, kila nchi memba inazo haki sawa na mawajibu sawa. Kwa kuwa sauti ya kila nchi iwe na bahati sawa ya kushiriki kwenye mabishano, kupata habari na mi-chango ya kutoa zinapashwa kuweza kufanyika kwa urahisi katika lugha zote rasmi.

Nguvu

Zikiwa zenye kuandikwa katika kiingereza kibovu, nyaraka zinapashwa, mara nyingi kusahihishwa na ofisi za tafsiri na zinabakia bila kuwa wazi sana na zisizoeleweka. Kuchua sauti katika lugha isiyoeleweka vizuri kunapoteza msingi wa fikra na kunailetea matatizo **kazi ya wafafanuzi**. Katika kazi ya kulinda amani, kuelewa vizuri lugha ya watu wanaohusika ni, bila shaka, jambo la nguvu.

Habari

Kupata habari kwa kinywa ao kwa maandishi zenye kutolewa katika lugha rasmi na ya kazi ni sharti muhimu kwa **kutimiza vizuri** kazi ya wafanyakazi, ya wakilishi na ya wajumbe wa

ofisi za kudumu. Kwani, wakati wa ufafanuzi, usikivu mbaya ao kutoelewana vinaweza kuwa chanzo cha mizozo.
Vilevile, ni muhimu kwa mashirika kutoa matangazo yao katika kutumia maneno kamili, sahihi, hasa kuhusu maswala makuu, na kulinda hivi kuweko mazungumzo kati ya tamaduni.

Mawasiliano

Kila mfanyakazi, mwakilishi ao mjumbe anayo haki ya kujieleza **katika lugha inayo kuwa rahisi kwake** ikiwa kama taratibu za lugha ya shirika zinakubali matumizi yake. Kuchagua lugha ya mawasiliano kunaweza kuchangia katika uwezo wa kujieleza, wa kueleweka na wa kutetea kwa nguvu maoni na faida za mtu ; wakati huyu anatumia lugha nyingine isiyo kuwa ile ya mama, ao ile lugha ya kigeni anayoielewa vizuri zaidi, inambidi kurahisisha na kuondoa mifumo midogomidogo katika fikra yake na ginsi ya kuieleza. Matendo haya yanaharibu kidogo mesali yake.
Urahisi na usahihi wa kutoa maneno ni masharti muhimu ili kuweko **mazungumzo ya hali** ya juu katika mazingira ya kazi, na hasa kwa wafanyakazi na mabalozi.

Mazungumzo na mapatano

Matumizi ya lugha moja yanapunguza pia kwa ofisi za kimataifa uwezekano wa kutoa maoni, uamzi na hila tofauti (za kutokana na tamaduni nyingi) juu ya kukabiliana na matatizo ya changamoto zinazopashwa kutatuliwa.

Desturi Nzuri

Tatizo siyo matumizi ya kiingereza, lakini kutawaliwa na lugha moja kwa kisingizio, *cha uongo!*, cha kutaka kurahisisha mawasiliano.

Lengo ni kutaka kutiwa usawa wa nguvu kati ya lugha rasmi na ya kazi ya mashirika ya kimataifa.

Mabalozi na wafanyakazi ni watendaji wakubwa katika kuhamasisha watu juu ya matumizi ya lugha nyingi.
Kusema kweli, lugha siyo lengo la mawasiliano, bali ni chombo bora kinachoruhusu kusafirisha fikra na mtazamo wa pekee kuhusu ulimwengu na changamoto kubwa za mambo mapya ya kimataifa.

Kuhusu tafsiri na ufafanuzi

Wakati wa mikutano rasmi

Kuyapatia mazungumzo hali ya kidemokrasia na ya nguvu

Ni vema kila mjumbe ajieleze katika moja ya lugha rasmi za nchi yake ao katika lugha rasmi ya shirika anayoielewa vizuri zaidi.

Watafsiri pamoja na wafafanuzi, wanaotakiwa kuweko katika mikutano hiyo, wanashutumu hasa desturi inayotawanyika sana ya kutoa nyaraka ao kuchukua sauti katika kiingereza, mara nyingi kibovu.
Usahihi wa mazungumzo unateseka na gharama ya ziada kuhusu kazi ya kukagua /kusahihisha nyaraka zinazotumwa kunako ofisi za Mikutano zinaongezeka mwaka kwa mwaka.

Ikiwa lazima, haifai kusita juu ya :

Kuhairisha uchukuzi wa uamzi, wa kauli ao kusudio lolote ikiwa kama nyaraka hazipo tayari katika lugha zote za kazi ;

Kuomba kuhairisha mkutano wakati tafsiri ya nyaraka za mwanzo, maandishi rasmi ao ripoti za mikutano ya awali azipo ;

Kuchunguza vizuri kama nyaraka kuhusu pwenti zinazostahili kuzungumziwa katika mkutano zimejulishwa katika lugha za kazi ;

Kumjulisha mratibu mwenye kuhusika na matumizi ya lugha nyingi ao kunako ofisi yenye kuhusika ikiwa kama nyaraka ao ripoti moja haipo tayari katika lugha rasmi za shirika ;

Kupinga kunako ofisi yenye kuhusika ikiwa kama habari moja iliyotangazwa kunako mtandao wa inteneti wa shirika imetolewa tu katika lugha moja.

Wakati wa mikutano isiyo rasmi

Kujaribu kutia uwelewano wa kila upande, kuchagua urahisi na usahihi.

Kuzidishwa mikutano isiyo rasmi katika lugha moja kunaharibu mwendesho wa demokrasia na kunahatarisha uwakilisho wa mashirika katika kuchangia juu ya **kupunguza kiwango cha kupata habari** kutokana na uwezo wa kuelewa kikweli lugha fulani wa wale wanaozungumza.

Haifai kusita

Kushutumu kutokuwepo ufafanuzi wa moja kwa moja wakati wa mkutano unaoangaliwa kama usiyokuwa rasmi, lakini ambao, kikweli, hali yake ni karibu sawa na ile ya kitaasisi ;

Kuchukua sauti katika lugha yako ao katika (z)ile lugha rasmi unayoielewa vizuri ;

Kuzilazimisha ofisi zenye kuhusika tafsiri za nyaraka zilizochunguzwa katika lugha rasmi za shirika ;

Kuhusu mikusanyiko ya kiufundi, kuchukua mpango wa kuifanya kutokana na makundi yanayopatana na maeneo ya lugha, hasa kuhusu maswala maalum.

Kuhusu kuwaandikisha watu kazini

Kuepuka ubaguzi katika kuwaandikisha watu kazini

Kwa desturi, wakati wa kuwaandikisha watu kazini katika mashirika ya kimataifa, uelewaji wa lugha moja miongoni mwa zile za kazi unalazimishwa ; lakini, kusema kweli, ni uelewaji wa kiingereza, peke yake tu, ndiyo unaolazimishwa.

Na vilevile, taratibu kubwa za kuandikishwa kazini zinafanyika katika kiingereza ; desturi hii inawapatia bahati kubwa wale wanaotumia lugha hii tangu kuzaliwa kwao na inazidisha kuimarika mwelekeo kunako matumizi ya lugha moja tu.

Matendo halisi yanayoweza kufanywa :

Kudai zitangazwe, moja kwa moja, kwa kupitia njia na lugha zote za kazi nafasi zinazo kuwa tupu ;

Kuangalia vizuri ya kama katika viti maalum (kiongozi, mkurugenzi wa tawi, spika), watakaokubaliwa kazini wawe na uweleo mzuri na wa kweli wa lugha mbili za kazi, kwa uchache, ao wahaidie kuzifunza ;

Kuchunguza kama kamati ya uchaguzi inayohusika na mazungumzo inatungwa na watu wanaotumia lugha nyingi ; na vilevile kama matumizi ya lugha nyingi za kazi/rasmi yatachunguzwa kikweli wakati wa mazungumzo kwa kuwaandikisha watu kazini ;

Kuwakumbusha watu wanaotaka kuandikwa katika kazi ya kulinda usalama umuhimu wa kuwa na uwezo wa kuzungumza katika lugha rasmi ya nchi ambako wanapashwa kutumika ;

Kutilia mkazo ili Mwakalishi mkaaji wa Programu ya Umoja wa mataifa kuhusu maendeleo ambaye pia ni mratibu wa

kazi zote za vituo vya Umoja wa mataifa katika eneo fulani, kunako nchi shirika, awe na ujuzi wa kweli wa lugha kubwa ya nchi anakostahili kutumwa.

Kuhusu mawasiliano na habari

Kuwaelekeza watu wote

Kulazimisha ofisi ya uandishi itume matangazo na barua katika lugha ya balozi anayehusika ; huyu, kwa zamu yake, atairudisha kunako ofisi ya uandishi katika lugha atakayoichagua ;

Kufanya yote ili mesali za simu na za mtandao wa inteneti za kutoka kwa wajumbe wa kitaifa ziwe katika moja ya lugha rasmi za nchi yao ;

Kujulishwa ukosefu wa usawa katika mtandao wa inteneti kati ya yale yanayoelezwa katika kiingereza na yale yanayojulishwa katika lugha nyingine za kazi ;

Kudai alama, mabango na matangazo kunako mahali pa kazi yafanyiwe katika lugha zote rasmi.

Katika matendo ya pamoja

Kutenda katika ngazi zote

Matumizi ya lugha nyingi yanaangaliwa kama kanuni kubwa katika nyaraka (kusudio la baada ya myaka miwili la Umoja wa mataifa, kanuni kunako Umoja wa Ulaya, Azimio la kikatiba la Umoja wa Afrika…), lakini inatakiwa **watu wote wapiganie** hiyo.

Kuwezesha yatungwe makundi ya kilugha ndani ya mashirika ya kimataifa, ginsi ilivyo kwa mabalozi wanaotumia lugha ya kifaransa ;

Kudai ifanyiwe mipango ya mafunzo na usaidizi wa kilugha kwa viongozi wake wa kitaifa ;

Kupinga kwa kukataa mipango ya kiuchumi inayo kuwa na vinyume vibaya kuhusu nafasi na matumizi ya lugha rasmi na za kazi ;

Kutumika katika ushirikiano wa karibu na wakilishi wa maeneo yote ya kilugha ndani ya mashirika ya kimataifa ao ya kimkoa juu ya kuheshimisha kanuni za kuweko tofauti za tamaduni na lugha, pia na hali ya lugha.

Katika ofisi za kuchua uamzi

Kuutilia mkazo uamzi

Katika kila shirika, zaidi ya mikutano ya kawaida kuhusu bajeti, ni vema kuweko ofisi kadha za uamzi ambazo zingeliweza kutumika kwa kutetea na kukuza matumizi ya lugha nyingi ginsi ilivyo, kwa mfano, kunako Umoja wa mataifa :

Kamati ya habari, mkutano wa kila mwaka unayozungumzia maswala yote yanayoelekea habari na mawasiliano. Uamzi utakaotoka katika kazi za kamati hiyo unao mipango mingi yenye matukio kuhusu matumizi ya lugha nyingi. Basi ni lazima kutopuuza ofisi hii. Uamzi huu, wa kila mwaka, unakuja kukamilisha ule wa baada ya myaka miwili kuhusu matumizi ya lugha nyingi, uliokubaliwa na Baraza kuu linalorudilia, kwa kirefu, mipango mingi.

Kamati ya mikutano mnamoshiriki Nchi memba 23 na inayokusanyika kwa muda wa juma moja mwanzoni mwa kila mwezi wa septemba. Kamati inakubali mipango mikubwa inayokuwa na matukio ya moja kwa moja juu ya ufafanuzi na tafsiri ; na itakuwa lazima watetezi wa matumizi ya lugha nyingi washiriki katika mkutano huo, hata kama wangalizi tu.

Mikutano ya kukadiria hali, ambayo inafanyiwa na ofisi za lugha. Mikutano hiyo, inayofanyika mara mbili mwakani, inayo lengo la kukusanya kutokea kwa Nchi memba maoni yao kuhusu kuboreshwa kwa ofisi za lugha.

Uamzi kuhusu mwendesho wa watu ambao unakubaliwa mara mbili mwakani na unaozungumzia maswala yanayohusika na kuwaandikisha watu kazini, mafunzo na usafirishaji wao ambao unao na upande fulani wa kilugha.

HABARI ZA MANUFAA

- Siku za lugha
- Mawasiliano
- Mfumo wa lugha wa mashirika makubwa ya kimataifa
- Nchi na serkali memba za Francofonia
- *Mwongozo* wa Francofonia Kuhusu matumizi ya lugha ya kifaransa katika mashirika ya kimataifa

Siku za lugha kunako Umoja wa mataifa

© United Nations

Siku za lugha kunako Umoja wa mataifa ziliingizwa mnamo mwaka wa 2010 sababu ya kukuza katika usawa matumizi ya lugha nyingi na tofauti za kitamaduni na pia matumizi ya lugha sita rasmi za Shirika. ofisi za Umoja wa mataifa, ulimwenguni, zinasherehekea siku sita maalum zinazopatana kila moja na lugha rasmi : **kifaransa (marsi 20), kichina (aprili 20), kiingereza (aprili 23), kirusi (juni 6), kihispania (oktoba 12) na kiarabu (disemba 18)**.
http://www.un.org/fr/events/observances/days.shtml

Siku ya kimataifa ya Francofonia

Tangu mwaka wa 1990, wanafrancofonia wa mabara yote wanasherehekea kila tarehe **20 Marsi** kama siku ya kimataifa ya Francofonia. Ni, tarehe ile, kote ulimwenguni wanafrancofonia wanahakikisha mshikamano na nia yao ya kuishi pamoja katika tofauti na umbalimbali. Tarehe ile imechaguliwa kwa kukumbuka kutiliwa mkono, mnamo mwaka wa 1970 pale Niamey (Nijeri), mkataba kuhusu kuanzishwa Ofisi ya ushushirikiano wa kitamaduni na kiufundi (ACCT), unaojulikana leo kwa jina la Shirika la kimataifa la Francofonia.
http://www.20mars.francophonie.org/

Siku ya Ulaya ya lugha

Kutokana na nia ya Baraza la Ulaya, siku ya Ulaya ya lugha inasherehekewa kila mwaka mnamo tarehe **26 septemba** tangu mwaka wa 2001. Mamia ya shuruli kote Ulaya zinasherehekea kuweko tofauti za lugha na zinasaidia katika kufunzwa kwao, kwani « kusherehekea lugha kunamaanisha kusherehekea tofauti za kitamaduni ».
www.coe.int/EDL

Siku ya kimataifa ya lugha ya mama

Katika mwaka wa 1999, tarehe **21 februari** ilitangazwa na UNESCO kama siku ya kimataifa ya lugha ya mama. Utamaduni wa amani unaweza kujengeka katika eneo ambamo watu wote wana haki ya kutumia kabisa katika uhuru mkubwa lugha ya mama katika nyakati zote za maisha. « Kutambua na kuheshimu tofauti za kitamaduni katika uwanja wa lugha kunaleta mshikamano ambao misingi yake ni uwelewano, kuvumiliana na mazungumzo ; na kila jambo linalowezesha matumizi ya lugha za mama litumike siyo tu kwa kusaidia kuweko tofauti za kilugha na kuelimisha katika lugha nyingi, lakini itusaidie zaidi kukubali kuweko, ulimwenguni, lugha na tamaduni nyingi. »
http://www.un.org/fr/events/culturaldiversityday/

Siku ya ulimwengu ya tofauti ya kitamaduni kwa mazungumzo na maendeleo



Tarehe 2 novemba 2001, UNESCO ilikubali Azimio lake la kiulimwengu kuhusu tofauti za kitamaduni. Kwa mara ya kwanza, Azimio hili lilitambua kuweko tofauti za kitamaduni kama « urisi wa pamoja wa binadamu » na kulindwa kwake kama sharti wazi na ya hali ambayo havipashwi kutenganishwa na heshima ya utu. Kutokana na ile, Baraza kuu la Umoja wa mataifa lilitangaza tarehe **21 Mayi**, kama siku ya ulimwengu ya kuweko tofauti za kitamaduni juu ya mazungumzo na maendeleo ili kuchunguza kwa undani fikra kuhusu samani za tofauti za kitamaduni na nia ya kujifunza vizuri zaidi « kuishi pamoja ».
http://portal.unesco.org

WARATIBU JUU YA MATUMIZI YA LUGHA NYINGI NDANI YA MASHIRIKA YA KIMATAIFA

- **Mratibu juu ya matumizi ya lugha nyingi kunako Ofisi za Umoja wa mataifa za uandishi.**
  Bwana Peter Launsky-Tieffenthal
  Makamu Katibu mkuu kuhusu Mawasiliano na Habari
  Wizara ya Habari, Umoja wa mataifa
  NY 10017, New York , États-Unis

- **Mratibu juu ya matumizi ya lugha nyingi kunako ofisi ya Umoja wa mataifa pale Geneva**
  Bwana Zhengren Li
  Tawi la ofisi za Mikutano
  Ofisi ya Umoja wa mataifa, 1211 Genève 10.
  Baruapepe : zli@unog.ch

- **Mratibu juu ya matumizi ya lugha nyingi kunako Shirika la Ulimwengu kuhusu Afia**
  Dr. Hooman Momen, *Mratibu wa Habari*
  20, Barabara Appia.1211 Genève 27
  Baruapepe : momenh@who.int

- **Kamisa wa Ulaya juu ya Elimu, utamaduni, matumizi ya lugha nyingi na vijana**
  Bibi Androulla Vassiliou
  Rue de la loi 200.BERL 10/110
  B-1049 Bruxelles
  Baruapepe : androulla.vassiliuo@ec.europa.eu

- **Mratibu kuhusu kifaransa, Tume ya Umoja wa Afrika.**
  Bwana Thomas Tschiggfrey
  Ofisi ya Makamu Prezidenti
  Tume ya Umoja wa Afrika
  S.L.P. 3243 Addis-Abeba, Éthiopie
  Baruapepe :TschiggfreyT@africa-union.org

Mfumo wa lugha
wa mashirika makubwa ya kimataifa

Mashirika	Lugha rasmi	lugha za kazi
Baraza kuu la Umoja wa mataifa Kanuni za ndani, kip., 51 (A/520/Rev.15)	Kiingereza, kiarabu, kichina, kihispania, kifaransa, kirusi	kiingereza, kiarabu, kichina, kihispania, kifaransa, kirusi, Ofisi za katibu mkuu kifaransa na kiingereza
Benki kuu la Dunia (BM)	haijulishwi	kiingereza Tafsiri kiarabu, kihispania, kifaransa, kimandarini, kireno, kirusi
Tume ya kiuchumi juu ya Afrika ya Umoja wa mataifa (CEA) Kanuni za ndani, kip.31-35 (E/CN.14/111/Rev.8/Corr .21)	kiingereza, kiarabu, kifaransa	kiingereza, kiarabu, kifaransa
Jumuiya ya kiuchumi ya Nchi za Afrika ya magharibi (CEDEAO)	kiingereza, kifaransa, kireno	kiingereza, kifaransa, kireno
Baraza la kimataifa la sheria (CIJ) Daraja ya 1945, kip. 39.1.	kiingereza, kifaransa	kiingereza, kifaransa
Baraza la Umoja wa mataifa kuhusu biashara na maendeleo (CNUCED) kanuni za ndani, kip.69 (ITD/63/Rev.) na kip. 64 (TD/B/740)	kijerumani, kiingereza, kiarabu, kichina, kihispania, kifaransa, kirusi	Ofisi ya uandishi kiingereza, kifaransa
Baraza la usalama la Umoja wa mataifa Kanuni za ndani, kip. 41 (S/96/Rev.7)	kiingereza, kiarabu, kichina, kihispania, kifaransa, kirusi	kiingereza, kiarabu, kichina, kihispania, kifaransa, kirusi
Baraza la kiuchumi na kijamii la Umoja wa mataifa (Ecosoc) Kanuni za ndani, kip. 32 E/5715/Rev.2 na E/5975/Rev.1 kuhusu tume za kiufundi	kiingereza, kiarabu, kichina, kihispania, kifaransa, kirusi	kiingereza, kihispania, kifaransa

Mashirika	Lugha rasmi	lugha za kazi
Fuko la fedha la kimataifa (FMI) Kanuni, kip. C13	Haijulishwi	kiingereza Tafsiri kijerumani, kiarabu, kichina, kihispania, kifaransa, kireno, kirusi
Shirika la ushirikiano na maendeleo ya kiuchumi (OCDE) Mkataba wa 14 disemba 1960	kiingereza, kifaransa	kiingereza, kifaransa
Shirika la kimataifa la o vya angani (OACI) Kanuni za ndani za Baraza kuu, kip. 64 na 65 na kanuni za ndani za Baraza, kip.56	kiingereza, kiarabu, kichina, kihispania, kifaransa, kirusi	kiingereza, kiarabu, kichina, kihispania, kifaransa, kirusi
Shirika la Umoja wa mataifa kuhusu chakula na kilimo (FAO) Kanuni kuu, Kip.XLVII	kiingereza, kiarabu, kichina, kihispania, kifaransa	kiingereza, kiarabu, kichina, kihispania, kifaransa
Shirika la kimatifa kuhusu hajira (OIT) Kanuni za Baraza la kimataifa kuhusu kazi, kip.24 na 58	kiingereza, kifaransa (mikutano na Tume)	kiingereza, kihispania, kifaransa, Tafsiri kijerumani, kiarabu, kichina, kirusi
Shirika la kiulimwengu kuhusu biashara (OMC)	kiingereza, kihispania, kifaransa	kiingereza, kihispania, kifaransa
Umoja wa Ulaya (UE) CE kanuni za ndani, kip. 1, Mkataba uliotia CE	kijerumani, kiingereza, kibulgaria, kidachi, kihispania, kiestonia, kifinwa, kifaransa, kigiriki, kihongria, kirlandi, kiitaliano, kiletoni, kilituani, kimalta, kiholanzi, kipolanzi, kirumania, kislovakia, kistovenia, kiswidi, kitcheki Kunako kamisheni kijerumani, kiingereza, kifaransa	kijerumani, kiingereza, kibulgaria, kidachi, kihispania, kiestonia, kifinwa, kifaransa, kigiriki, kihongrwa, kirlandi, kiitaliano, kiletoni, kilituani, kimalta, kiholanzi, kipolanzi, kirumania, kislovakia, kistovenia, kiswidi, kitcheki Kunako Tume kijerumani, kiingereza, kifaransa

Mashirika	Lugha rasmi	lugha za kazi
Shirika la kiulimwengu la mali ya akili (OMPI) kip. 6 na 2 na VII vya mktaba uliotia OMPI na Baraza kuu la Nchi memba	kiingereza, kiarabu, kichina, kihispania, kifaransa, kirusi	kiingereza, kiarabu, kichina, kihispania, kifaransa, kirusi
Shirika la kiulimwengu kuhusu afia (OMS) Kanuni za ndani za Baraza la utendaji n kip. 22, AG na Baraza la utendaji	kiingereza, kiarabu, kichina, kihispania, kifaransa, kirusi	kiingereza, kiarabu, kichina, kihispania, kifaransa, kirusi
Umoja wa Afrika (UA) Sheria ya kikatiba, kip.25, kanuni za ndani za Baraza, kip. 14, kanuni za ndani za Baraza la utendaji, kip.15 na kanuni za ndani za Kamati ya wakilishi wa kudumu, kip. 10	kiingereza, kiarabu, kihispania, kifaransa, kireno, kiswahili, lugha yoyote ya kiafrika	kiingereza, kiarabu, kihispania, kifaransa, kireno
Umoja wa kimataifa telecommunications (IUT) Baraza la Nice (1989) na Makusudio 103 na COM 6/1 ya mabaraza ya Minneapolis (2002) na Marrakech (1998)	Haijulishwi	kiingereza, kiarabu, kichina, kihispania ; kifaransa, kirusi
Shirika la Umoja wa mataifa kihusu elimu, sayansi na utamaduni (Unesco) Kanuni za ndani za Baraza kuu, kip. 50, 54 na 55 na kanuni za ndani za Baraza la utendaji, kip. 21.	Baraza kuu kiingereza, kiarabu, kichina, kihispania, kifaransa, kihindi, kiitaliano, kireno, kirusi.	Baraza na Mkutano wa utendaji kiingereza, kiarabu, kichina, kihispania, kifaransa, kirusi, Ofisi ya uandishi kiingereza, kifaransa

Nchi na Serkali memba za Francofonia

Likipatikana katika mabara matano, Shirika la kimataifa la Francofonia linazikusanya **nchi na serkali 77** ; **57 zikiwa memba** na **20 wangalizi**.

Nchi na Serkali makumi matano na saba, memba na shirika

Albania • Andore • Armenia-Ubelgiji • Benini • Bulgaria • Bukinafaso • Burundi • Cambojia • Kameruni • Canada • Canada-Nouveau-Brunswick • Canada-Québec • Cap vert • Chypre* • Congo • Kodivaa • Djibouti • Dominika • Misri • Jamuhuri ya zamani ya Yugoslavia ya Masedonia • Shirikisho la Wallonie-Bruxelles • Ufaransa • Gaboni • Ghana* • Ugiriki • Gine • GineBisau • Ginekweta • Haiti • Laosi • Lebanoni • Luxembourg • Madagaska • Mali • Moroco • Morisi • Moritania • Moldavia • Monaco • Nijeri • Qatar* • Jamuhuri ya Afrika ya kati • Jamuhuri ya kidemokrasia ya Congo • Rumania • Rwanda • Sainte Lucie • Saotome na Prinsipe • Senegali • Ushelisheli • Uswisi • Chadi • Togo • Tunisia • Vanuatu • Vietanamu.

*memba shirika

Wangalizi makumi mawili

Autriche • Bosnia • Herzegovina • Croatia • Umoja wa Falme za kiarabu • Estonia • Georgia • Hongria • Lettonia • Lituania • Montenegro • Msumbiji • Upolanzi • Jamuhuri ya Dominiki • Jamuhuri ya Tcheque • Serbia • Slovaquia • Thailande • Ukraina • Uruguay.

Mwongozo wa Francofonia

Kuhusu matumizi ya lugha ya kifaransa katika mashirika ya kimataifa

Mwongozo uliyokubaliwa na Nchi memba, shirika na wangalizi wa OIF katika kikao cha 22 cha Baraza ya mawaziri wa Francofonia mnamo mwaka wa 2006, ni matukio maalum ya fikra ya kisiasa ; unajulisha **mapiganio ya hali na kisheria ya Nchi kuhusu kuwezesha matumizi ya kifaransa katika mashirika ya kimataifa kwa sababu ya kuendelesha matumizi ya lugha nyingi**.

Sisi, mawaziri walioshiriki kunako Baraza la Francofonia, lililofanyika Bucaresti, tarehe 26 septemba 2006 ;

Tukiguswa na matatizo yanayotukia katika matumizi ya kifaransa katika mikutano ya mashirika ya kimataifa na ya kimkoa ;

Tukilitilia mkazo pendo letu kuhusu kuweko tofauti za tamaduni na lugha, kuhusu heshima kubwa ya hali ya lugha ya kazi ao lugha rasmi zinazotambuliwa na nyaraka za ofisi za mashirika ya kimataifa na ya kimkoa ambamo Nchi na serkali ni memba ;

Tukikumbusha ya kwamba kifaransa ni moja miongoni mwa lugha mbili za kazi za Umoja wa mataifa na taasisi zake maalum ;

Katika mashirika ya kimataifa na ya kimkoa ambamo kifaransa kinapatiwa hali ya lugha ya kazi ao lugha rasmi, pamoja na wakilishi na wajumbe tunapigania juu ya :

➜ kujieleza katika kifaransa kama hii ni lugha yetu peke ya kitaifa ao rasmi ;

➜ kutia usawa katika matumizi ya kifaransa ikiwa kama nchi yetu inazitambua lugha nyingi za kitaifa ao rasmi, kwa kuonyesha hivi tofauti ya kiutamaduni ;

➜ kupendelea kujieleza katika kifaransa katika nyakati nyingine zote ambamo haiwezekani kutumia lugha yetu ao ya lugha zetu za kitaifa ao rasmi, tofauti na kifaransa ;

Na tena, kujikaza, wakati wa mabaraza makuu na vikao vya mawaziri, ikiwa kama hatutumii kifaransa, wakati wa kugawa nyaraka, tafsiri za kifaransa zitolewe pia na ofisi ya uandishi shirkia ao na ujumbe wetu ikiwa kama inakusudiwa kugawanya maandishi.

Zaidi, tunakusudia kwa wakilishi na wajumbe wetu kunako mashirika haya :

1) ifanyike kunako jopo la waandishi la mashirika ufafanuzi wa moja kwa moja wa mambo yanayozungumziwa wakati wa vikao rasmi na katika nyakati maalum za uchunguzi wa maandishi ; kusiwe mikutano mingi mno bila ufafanuzi ;

2) Kuchunguza ili :

➜ Kila nyaraka na matangazo, hata yale kwa njia ya eletroniki, yapatikane pia katika kifaransa ao, ikiwa kuna tafsiri, katika kifaransa cha hali ya juu, kinachopatana na nyaraka halisi ;

➜ Maandishi maalum kuhusu mapatano yanapashwa pia kupatikana, bila kukawia, katika kifaransa ;

3) Kutoa, katika majopo ya mabalozi wanaotumia kifaransa, mashauri kwa kuwezesha matumizi ya kifaransa na kupinga kunako jopo la waandishi, ikiwa lazima kwa pamoja, kunakosea katika kutekeleza kanuni juu ya matumizi ya lugha nyingi ;

4) Kushurlika na malipo ya mashirika haya ya mali na watu yanayostahili juu hali ya lugha za kazi ao lugha rasmi ziheshimike kimatendo :

5) wachangie, kwa pamoja, ili mashirika yatumie kabisa matumizi ya lugha nyingi kama sharti kwa kuwaandikisha watu kazini.
6) Wachangie ili, katika kazi ya kulinda amani inayofanyiwa kunako eneo moja kunakotumiwa kifaransa, majeshi ya shirika la kimataifa ao la kimkoa yenye kuhusika yaweze kuwasiliana na viongozi na raia katika kifaransa ; na ikiwa izingatiwe katika kuwaandikisha watu kazini na kuwapatia mafunzo wafanyakazi wa kazi za kulinda amani ;
7) Watumike pamoja na mawakilishi wa makundi mengine ya lugha zinazotambuliwa katika mashirika ya kimataifa na ya kimkoa, kwa kuheshimisha taratibu za matumizi ya lugha nyingi na kuweko tofauti za kitamaduni pamoja na hali ya lugha za kazi na lugha rasmi.

Kwa hiyo, tunayazingatia makusudio yaliyochukuliwa ndani ya mashirika haya juu kuwezesha kufundisha lugha kwa wafanyakazi na tunasimamia matendo yanayofanywa na OIF juu ya kufundisha kifaransa kwa wafanyakazi wa mashirika haya na nchi na serkali memba ambao kifaransa si lugha yao rasmi ; tutafikiria pamoja tena juu ya kuwezesha kuwaandikisha kazini watu ambao wanaelewa kifaransa kunako viti vya uongozi ndani ya mashirika.

Tunamuomba Katibu Mkuu wa Francofonia kuongeza kabisa mapiganio yake kuhusu matumizi ya kifaransa katika mashirika ya kimataifa, hasa kwa kupitia ofisi za uwakilishi wa kudumu za OIF na matendo mengine ya usaidizi tutakayoangalia kama yenye kutakiwa.